GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6649 **20 Aprili, 2017** **Bei, Shs.3,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo..... 125

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 10 Mei, 2017 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
20 Aprili, 2017

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

wa

SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 3 YA 1985 NA KUANZISHA UPYA MAHAKAMA YA KADHI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya 2017 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Kadhi" maana yake ni Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Rufaa na Kadhi wa Wilaya;

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar;

"Kadhi Mkuu" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii kuwa kiongozi mkuu wa Mahakama ya Kadhi;

"Mahakama ya Kadhi" inajumuisha Mahakama ya Kadhi wa Wilaya na Mahakama ya Kadhi wa Rufaa;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahakama ya Kadhi aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Sheria ya Kiislamu" maana yake ni mfumo wa Sheria ya Kiislam ambao msingi wake ni Sheria za Kiislam;

"Ulamaa" maana yake ni mtu mwenye taalauma ya dini ya kiislam, aliyeteuliwa kuwa Ulamaa chini ya Sheria ya Ofisi Mufti Na. 9 ya 2001;

"Vakili" maana yake ni mtu aliyeruhusiwa na mwenye leseni ya kufanya kazi ya Uvakili katika Mahakama ya Kadhi na Mahakama ya Mwanzo, chini ya masharti Sheria inayosimamia mfumo unaoruhusu watu kufanyakazi za uwakili;

"Tume ya Utumishi" maana yake ni Tume ya Utumishi ya Mahakama iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 102 cha Katiba ya Zanzibar yam waka 1984;

"Wakili" maana yake ni mtu yeyote ambaye si Vakili, aliyeruhusiwa kufanya kazi ya uwakili Mahakama Kuu ya Zazibar na Mahakama zilizo chini yake, kwa mujibu wa masharti ya Sheria inayosimamia mfumo unaoruhusu watu kufanya kazi ya uwakili;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo ya sheria.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA, MUUNDO, MAMLAKA NA USIMAMIZIWA MAHAKAMA ZA KADHI

Kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi.

3.-(1) Kunaanzishwa Mahakama ya Kadhi.

(2) Mahakama ya Kadhi itaundwa na Mahakama ya Kadhi wa Wilaya na Mahakama ya Kadhi wa Rufaa.

(3) Mahakama ya Kadhi wa Wilaya itakuwa na mamlaka ya awali ya kusikiliza kesi za madai kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 5 cha Sheria hii.

Muhuri wa Mahakama.

4. Mahakama za Kadhi zitakuwa na muhuri utaokuwa na sura ya kiMahakama na muundo mwengine wowote utakaoridhiwa na Jaji Mkuu.

Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi.

5.-(1) Mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo Wadaawa ni Waislam kuhusiana na:

(a) Ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa;

(b) ustawi wa familia;

(c) matunzo na malezi ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa;

(d) huduma na misaada;

(e) Wakfu au amana za kidini, hiba na mirathi;

(f) wasia;

(g) jambo jengine lolote ambalo Mahakama ya Kadhi imepewa mamlaka na Sheria nyengine yoyote kulishugulikia.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki, mtu yeyote ambaye si Muislam anaweza kufungua shauri katika Mahakama ya Kadhi dhidi ya Muislamu kwa mashauri ya madai yanayohusu sheria ya Kiislam.

(3) Kila Kadhi atakuwa na mamlaka ya kusikiliza kosa lolote la kudharau Mahakama lilofanywa kuhusiana na ofisi yake na atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu kwa mujibu wa Sheria hii na Kanuni zilizotungwa kwa ajili hiyo.

Sheria ya Ushahidi.

6. Sheria na Kanuni za ushahidi zitakazotumika katika Mahakama za Kadhi zitakuwa ni zile tu zinazotumika katika Sheria ya Kiislam.

Kanuni za Taratibu na Utendaji kazi.

7. Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi Mkuu atatunga Kanuni za Mahakama ataandaa kanuni za utaratibu na utendaji kazi utakaotumika katika Mahakama ya Kadhi.

Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi

8.-(1) Kutakuwa na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa.

(2) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake atakula kiapo mbele ya Rais.

(3) Kadhi Mkuu atakua ndiye Mkuu wa Mahakama ya Kadhi na atakua na wajibu wa usimamizi wa mambo yote ya Mahakama ya Kadhi.

(4) Naibu Kadhi Mkuu atakuwa ndiye mshauri mkuu wa wa Kadhi Mkuu na atafanya kazi nyengine kama atakavyopewa na Kadhi Mkuu.

(5) Mtu hatofaa kushika au kukaimu Ofisi ya Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu mpaka awe muumini na mfuasi wa dini ya Kiislam na:

(a) awe muadilifu na mwenye kuheshimika;

(b) awe na kiwango cha elimu angalau shahada ya kwanza ya sheria ya Kiislam kutoa chuo kinachotambulika; na

(c) awe na uzoefu wa angalau miaka mitano kuhusiana na masuala ya Sheria ya Kiislam au taaluma ya Usul fiqhi.

(6) Rais anaweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumteua Naibu Kadhi Mkuu kuwa Kaimu Kadhi Mkuu iwapo itatokea:

(a) nafasi ya Kadhi Mkuu itakuwa wazi; au

(b) Kadhi Mkuu yuko likizo au yupo nje ya Tanzania; au

(c) Kadhi Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yeyote.

(7) Mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Kadhi Mkuu, atapewa nguvu na madaraka kamili ya Kadhi Mkuu na atafanya kazi za Kadhi Mkuu mpaka atakapoteuliwa Kadhi Mkuu mpya au mpaka Kadhi Mkuu aliyekuwa likizo au aliyekuwa hawezi kufanya kazi atakapoweza na kurejea kazini.

Muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

9. -(1) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu atabaki katika nafasi yake mpaka atakapofikia umri wa miaka sitini amabpo anaweza kustaafu kwa hiari au miaka sitini na tano amabpo atastaafu kwa lazima.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Rais anaweza kuongeza muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kama atakavyoona inafaa.

Kadhi wa Rufaa.

10.-(1) Kutakuwa na Makadhi wasiopungua watatu wa Rufaa watakaoteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Baraza la Ulamaa.

(2) Kadhi wa Rufaa hatoanza kazi za ofisi yake mpaka ale kiapo cha utii na kiapo chengine cha utekelezaji wa kazi zake kama ilivyoelezwa na sheria.

(3) Mtu hatofaa kuteuliwa kuwa Kadhi wa Rufaa mpaka awe muumini na muumini na mfuasi wa dini ya Kiislam na:

(a) awe muadilifu, mwenye kuheshimika;

(b) awe na umri wa angalau miaka 40;

(c) awe na angalau shahada ya kwanza ya Sheria ya Kiislam kutoka katika Chuo kinachotambulika; na

(d) awe na uzoefu wa angalau miaka mitano kwa mambo yanayohusiana na sheria za kiislamu au Usul-fiqhi.

Kadhi wa Wilaya.

11.-(1) Kutakuwa na Kadhi wa Wilaya katika kila Wilaya ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupendekezwa na Jaji Mkuu.

(2) Kadhi wa Wilaya hatoanza kazi zake mpaka ale kiapo cha utii na kiapo chengine cha utekelezaji kazi zake mbele ya Jaji Mkuu, kama ilivyoeleza sheria.

(3) Mtu hatofaa kushikilia nafasi ya Kadhi wa Wilaya au kukaimu katika Ofisi hiyo mpaka awe mfuasi na muumini wa dini ya Kiislam na:

(a) awe muadilifu na anayeheshimika; na

(b) awe na angalau shahada ya kwanza ya Sheria ya Kiislam hutoka chuo kinachotambulika.

Mrajis wa Mahakama ya Kadhi.

12.-(1) Inaanzishwa Afisi ya Mrajis wa Mahakama ya Kadhi ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupendekezwa na Kadhi Mkuu.

(2) Mrajis wa Mahakama ya Kadhi atawajibika kusimamia utawala wa Mahakama za Kadhi zote.

(3) Mtu hatateuliwa kuwa Mrajis wa Mahakama ya Kadhi mpaka:

(a) awe ameteuliwa au ana sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi; na

(b) awe na uzoefu wa angalau miaka mitano katika shughuli za Mahakama.

Uwezo na kazi za Mrajis.

13.-(1) Mrajis wa Mahakama ya Kadhi atakuwa na uwezo wa kutekeleza kazi zifuatazo:

(a) kutekeleza baadhi ya uwezo na wajibu wa Kadhi, na kusoma hukumu ya Mahakama ya Kadhi kwa maelekezo ya Kadhi Mkuu;

(b) kutoa amri na kufanya shughuli za Mahakama ya Kadhi zikiwemo:

(i) kufungua rufaa, mapitio na marudio ya kesi;

(ii) kutoa na kutuma taarifa ya wito wa Mahakama;

(iii) kuahirisha kesi;

(iv) kushughulikia ombi linalohusu malipo ya hukumu kwa awamu;

(v) kuondoa na kurekebisha rufaa, mapitio na marudio; na

(vi) malipo ya gharama za kusimamia utekelezaji hukumu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kadhi Mkuu kwa kushauriana na Jaji Mkuu, atampangia kazi na kumpa uwezo wa kazi Mrajis wa Mahakama ya Kadhi.

(3) Mrajis wa Mahakama ya Kadhi ataendesha na kusimamia viapo kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah.

(4) Mrajis wa Mahakama ya Kadhi atakuwa na uwezo unaolingana na uwezo wa Mrajis wa Mahakama Kuu kuhusiana na rufaa, marudio na ombi litaloletwa kwa ajili ya kusajiliwa.

(5) Mtu yeyote asiyeridhika na amri yoyote ya Mrajis wa Mahakama ya Kadhi (isipokuwa usomaji hukumu au amri iliyopitishwa na Kadhi) anaweza kuomba kupinga amri hiyo kwa Kadhi wa Rufaa kwa njia ya maombi, yakiambatanishwa na kiapo kadiri itakavyokuwa.

(6) Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa, atakuwa na uwezo kufuatilia ombi la mtu yeyote aliyeathirika na ombi hilo, kutengua amri au uamuzi uliopitishwa na Mrajis wa Mahakama ya Kadhi, na kutoa hukumu au amri nyengine ya haki.

(7) Ombi lilifanywa chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, litawasilishwa ndani ya siku thelathini tokea amri au uamuzi kutolewa, au muda mwengine kama Kadhi Mkuu atavyoruhusu.

(8) Ombi hilo halitozuia kuendelea kusikilizwa kesi ya msingi au utekelezaji wa hukumu yoyote isipokuwa kama Mrajis wa Mahakama ya Kadhi, Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa ataamuru vyenginevyo.

Bajeti na Fedha za Mahakama ya Kadhi.

14. (1) Mahakama ya Kadhi itakuwa na Fungu lake la Bajeti amabamo mtaingizwa fedha zote zilizoidhinishwa au zitakazostahili kwa matumizi ya Mahakama ya Kadhi.

(2) Mlipaji Mkuu wa Serikali atateua afisa mhasibu kwa ajili ya Fungu la Bajeti ya Mahakama ya Kadhi na Mhasibu Mkuu atateua wafanyakazi wa kutosha kufanya kazi za kiuhasibu kwa ajili ya Fungu hilo.

(3) Fedha za Mahakama ya Kadhi zitajumuisha:

(a) fedha zilizozoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika kila mwaka wa fedha kwa ajili ya matumizi ya Mahakama ya Kadhi;

(b) misaada, michango na fedha nyengine zilizopokelewa na Mahakama ya Kadhi kutoka vyanzo vyengine vinavokubalika;

Lugha ya Mahakama ya Kadhi.

15.-(1) Mwenendo na kumbukumbu za mwenendo wa kesi zitakuwa kwa lugha ya Kiswahili.

(2) Endapo itatokea mdaawa si muelewa wa Kiswahili au ana ulemavu wa kuzungumza au ulemavu mwengineo unaomzuia kuifahamu lugha ya Mahakama, Mahakama itatumia mkalimani.

(3) Kabla ya kuanza kazi yake ya ukalimani, Mkalimani ataapa mbele ya Mahakama ya Kadhi au Mrajis wa Mahakama ya Kadhi.

Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

16.-(1) Kutakuwa na Mahakama ya Kadhi wa Rufaa ambayo itakuwa na mamlaka ya rufaa na mapitio kwa hukumu na maamuzi yanayotoka Mahakama ya Kadhi wa Wilaya.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa na mapitio, Mahakama ya Kadhi wa Rufaa itaundwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa.

(3) Katika kutekeleza mamlaka yake, Mahakama ya Kadhi wa Rufaa itakuwa na uwezo wa:

(a) kubadilisha na kutengua hukumu, maamuzi na amri zote za Mahakama yoyote ya chini yake;

(b) kuamuru kusikilizwa upya kwa kesi yoyote iliyosikilizwa na kutolewa uamuzi katika Mahakama yoyote iliyo chini yake;

(c) kurejesha kesi yoyote iliyosikilizwa na kuamuliwa katika Mahakama yoyote iliyo chini yake ikiwa na maelekezo ya mwenendo wa ziada kama Kadhi Mkuu atakavyoona inafaa.

Rufaa kutoka Mahakama ya Kadhi ya Rufaa.

17.-(1) Rufaa au marudio kutokana na hukumu yoyote ya Mahakama ya Kadhi wa Rufaa itafunguliwa Mahakama Kuu.

(2) Katika kutekeleza uwezo wake wa rufaa na marudio, Mahakama Kuu itaundwa na Jaji wa Mahakama Kuu na jopo la Washauri wanne wa Kiislam watakaojulikana wanaojuilikana kama ulamaa.

(3) Ulamaa watateuliwa na Mrajisi wa Mahakama ya Kadhi miongoni mwa watu watakaopendekezwa na Baraza la Ulamaa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, maamuziya Mahakama Kuu yatakuwa ya mwisho.

(5) Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hiki anatakiwa awe Muislam mwanamme.

(6) Katika kuteua washauri wa mahakama chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mrajis atazingatia madhehebu ya Wadaawa.

(7) Uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusiana na kesi za Mahakama ya Kadhi utapaswa kufuatwa na kuzingatiwa na Mahakama zote Kadhi, isipokuwa kwamba, katika kuitumia hukumu hiyo kama marejeo madhehebu ya Wadaawa yatazingatiwa.

(8) Wakati wa kushughulikia rufaa, Jopo la Mahakama Kuu linaweza kumualika mtu yeyote mtambuzi wa jambo linalohusika kama wataalam wa sheria

Mahakama ya Kadhi wa Wilaya.

18.-(1) Jaji Mkuu anaweza kuanzisha katika kila Wilaya ya Zanzibar Mahakama ya Kadhi wa Wilaya ambayo itakuwa na mamlaka ndani ya Wilaya ilipoanzishwa tu.

(2) Mahakama ya Kadhi wa Wilaya inaweza kufanya kazi zake sehemu yoyote kwenye eneo la mamlaka yake.

(3) Mahakama ya Kadhi wa Wilaya itaongozwa na Kadhi wa Wilaya.

Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi ya Wilaya.

19. Mahakama ya Kadhi wa Wilaya itakuwa na itatekeleza mamlaka ya asili ya kusikiliza na kuamua mambo yote na kesi, kama zilivyoorodheshwa katika kifungu cha 5 cha Sheria hii.

Rufaa.

20. Rufaa kutokana na maamuzi ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya zitapelekwa katika Mahakama ya Kadhi wa Rufaa.

SEHEMU YA TATU
USULUHISHI

Uwezo wa kutoa amri na maelekezo ya kumaliza kesi.

21.-(1) Bila ya kujali chochote katika Sheria hii, Mahakama ya Kadhi ya Wilaya inaweza ndani ya siku tano za kazi kuanzia tarehe ya kufunguliwa kesi, kwa uamuzi wake yenyewe, kumtaka Mdaawa yeyote au Wadaawa katika kesi kuhudhuria Mahakamani, ili Mahakama iweze kutoa amri kuhusu maombi ya muda yaliyofunguliwa au yanayokusudiwa kufunguliwa kwa ajili ya uendheshaji wa kesi kwa misingi ya haki, haraka na kwa gharama nafuu.

(2) Mahakama pia inaweza kuzingatia jambo lolote ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kutatua mambo au jambo lolote katika kesi au mwenendo wa kesi, na kuwataka Wadaawa kuwasilisha Mahakamani taarifa yoyote inayoonekana inafaa, na pia inaweza kutoa maelekezo yoyote yanayoonekana kuwa ni muhimu au yanafaa kwa ajili ya upatikanaji haki, utatuzi wa haraka wa kesi na unafuu wa gharama.

Uwasilishaji wa kesi kwa usuluhishi.

22.-(1) Iwapo kesi haijapata ufumbuzi chini ya sharti la kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 23 cha Sheria hii, Mahakama inaweza kuelekeza Wadaawa kuwasilisha kesi yao kwa ajili ya usuluhishi na baada ya kutoa maelekezo hayo, Mahakama itateua msuluhishi ambaye atapanga tarehe ya kuanza hatua za usuluhishi, isipokuwa kama Wadaawa kwa pamoja wamewasilisha tamko la kwamba usuluhishi hauhitajiki.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, msuluhishi atateuliwa miongoni mwa watu wenye kuheshimika, waadilifu na waelewa wa masuala ya dini ya Kiislamu na ambaye atakubaliwa na pande zote zinazohusika na shauri liliopo Mahakamani.

Kazi ya Msuluhishi.

23.-(1) Katika kufanya usuluhishi chini ya Sheria hii:

(a) Msuluhishi atawawezesha Wadaawa kupunguza ucheleweshaji wa kazi ya suluhishi, na atafanya usuluhishi wa haraka na kwa misingi ya haki;

(b) Msuluhishi atawezesha kuwepo mawasiliano baina ya wadaawa ili kuwasaidia katika kufikia suluhu inayokubaliwa na pande zote.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Msuluhishi:

(a) atapaswa, bila upendeleo kufanya kila linalostahiki kuwasaidia wadaawa katika kutatua mgogoro wao;

(b) anaweza, ikilazimika, kufanya mikutano ya pamoja au ya mtu mmoja mmoja, na anaweza kutoa mapendekezo ya kufikia suluhu;

(c) pale ambapo huduma ya mtaalamu inaweza kupatikana bila ya malipo au bila gharama, au pale ambapo huduma hiyo inaweza kupatikana kwa malipo, na Wadaawa wakakubali kulipa gharama hizo, Msuluhishi anaweza kupata ushauri wa mtaalamu katika vipengele vinavyohitaji utaalamu katika mgogoro huo na utaalamu huo utatolewa kwa uhuru na bila ya upendeleo.

(d) ataongozwa na misingi ya haki, usawa na misingi ya asili ya utaoaji haki, na atazingatia pamoja na mambo mengine, haki na wajibu wa wadaawa, na mazingira yaliyouzunguka mgogoro wenyewe;

(e) anaweza, katika hatua yoyote ya utatuzi wa mgogoro huo na katika hali ambayo ataona inafaa kuzingatia matakwa ya wadaawa, likiwemo ombi la maelezo kutoka upande wowote wa mzozo, kwa ajili ya utatuzi wa haraka wa mgogoro; na

(f) anaweza, katika hatua yoyote ya usuluhishi, kutoa mapendekezo kwa ajili ya utatuzi wa mgogoro.

(3) Pale ambapo Wadaawa wataafikiana wakati wa usuluhishi, Msuluhishi atayaweka maafikiano hayo katika maandishi na wadaawa watasaini hati ya maafikiano.

(4) Msuluhishi atawasilisha maafikiano hayo kwa Kadhi aliyepangiwa kesi inayohusika na usuluhishi huo.

Haki ya utatuzi wa hoja.

24.-(1) Mdaawa katika kikao cha usuluhishi atakuwa na haki ya kutatua hoja yoyote wakati wa kikao cha usuluhishi.

(2) Upande unaohitaji ridhaa ya upande mwengine kabla au baada ya kuanza kwa usuluhishi, utafanya mawasiliano na upande mwengine katika usuluhushi huo.

Usiri.

25. Mawasiliano yote katika vikao vya usuluhishi, nyaraka na kumbukumbu za usuluhishi yatachukuliwa kuwa ni siri, na baada ya hapo taarifa zozote zilizotolewa wakati wa usuluhishi hazitazingatiwa na hazitatumika kama ushahidi katika mwenendo wa kesi Mahakamani au juhudi nyengine za usuluhishi, isipokuwa kuhusiana na madai yaliyoletwa na mdaawa yeyote kutengua makubaliano ya suluhu kwa sababu ya udanganyifu.

Muda wa Usuluhishi.

26. Muda wa usuluhishi hautazidi siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kikao cha kwanza cha upatanishi na ukihitajika muda wa ziada, muda huo ni lazima ukubaliwe na pande zinazohusika na usuluhishi.

Kuondoa mgogoro katika usuluhishi.

27.-(1) Ikiwa haiwezekani kuendesha usuluhishi kutokana na upande mmoja kutohudhuria vikao vya usuluhishi bila ya sababu za msingi au kutokana na sababu nyengine yoyote iliyo nje ya uwezo wa Msuluhishi, Msuluhishi anaweza kuondoa mgogoro katika usuluhishi na kuurejesha Mahakamani.

(2) Upande wowote usioridhika na amri iliyotolewa na msuluhishi chini ya kifungu hiki unaweza, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya amri hiyo, kuwasilisha Mahakamani ombi la kutaka kurejeshwa tena kwa Msuluhishi shauri lililoondolewa hapo awali.

(3) Baada ya kuridhika kwamba ada na gharama za usuluhishi zimelipwa kikamilifu, Msuluhishi anaweza kutengua uamuzi wake wa awali wa kuachana na usuluhishi, na kwa ridhaa ya Wadaawa wote wanaohusika, atatoa taarifa ya kuendelea na usuluhishi.

(4) Wakati wa usuluhishi, pale ambapo Wadaawa wameafikiana, Msuluhishi ataweka maafikiano hayo katika maandishi na Wadaawa na Msuluhishi watasaini hati ya maafikiano.

Mwisho wa Usuluhishi.

28. Usuluhishi utamalizika endapo:

(a) Msuluhishi atakatisha vikao vya usuluhishi kwa kukosa ushirikiano kutoka kwa Mdaawa au Wadaawa, au Mdaawa au Wadaa wameshindwa kutii maelekezo ya usuluhisi; au

(b) Wadaawa watasaini makubaliano ya usuluhishi;

(c) Msuluhishi atatoa tamko baada ya kushauriana na Wadaawa kwamba kuendelea na usuluhishi haiwezekani au hakuna maslahi; au

(d) Wadaawa kwa pamoja watakubaliana kwamba usuluhishi usitishwe; au

(e) Mdaawa mmoja ametoa tamko kwa Msuluhishi na Mdaawa mwengine akakubali kwamba usuluhishi usitishwe.

Usuluhishi ukishindikana.

29. Iwapo mpaka kufikia mwisho wa usuluhishi hakuna muafaka uliofikiwa, kesi itarejeshwa kwa Kadhi aliyepangiwa kuisikiliza, ambaye ataendelea kusikiliza kesi kuanzia pale kesi ilipopelekwa kwa msuluhishi.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

Kudharau Mahakama ya Kdhi.

30.-(1) Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuanzisha mashtaka dhidi ya mtu yeyote kwa kudharau Mahakama, na kwenye mashtaka hayo inaweza kuamuru adhabu ya kifungo kisichopungua mwezi mmoja au faini isiyopungua shilingi laki mbili, kwa mtu atakayepatikana na hatia ya kosa hilo.

(2) Mtu yeyote ambaye:

(a) akiwa katika eneo ambalo kazi za Mahakama zinaendelea, au ndani ya eneo linalotumika kwa kazi hizo, ataonesha dharau kwa maneno au vitendo kuhusiana na kesi inayosikilizwa, au kwa mtu yeyote ambaye yupo kwenye eneo ambalo kesi inaposikilizwa;

(b) akiwa ameitwa kutoa ushahidi katika kesi iliyopo Mahakamani na akashindwa kuhudhuria au anahudhuria lakini anakataa kuapishwa au kutoa uthibitisho, au bila sababu inayokubalika kisheria anakataa kujibu swali au kutoa hati, au anabakia katika chumba cha Mahakama baada ya kuamriwa kuondoka katika eneo hilo;

(c) anasababisha, kuzuia au anasababisha usumbufu katika usikilizaji kesi;

(d) wakati shauri linaendelea, anatoa maneno au maandishi, yanayoweza kupotosha mwenendo wa kesi, au kumzuia mtu yeyote kwa maslahi au dhidi ya maslahi ya upande wowote wa kesi hiyo, au anadhalilisha mamlaka ya mtu yeyote ambaye kesi hiyo iko mbele yake;

(e) kinyume cha sheria, anajaribu kuingilia au kushawishi shahidi katika kesi ama kabla au baada ya kutoa ushahidi, kuhusiana na ushahidi huo;

(f) anafanya kitendo kingine chochote chenye nia ya kuonyesha dharau au kuharibu mwenendo wa kesi, au kwa mtu yeyote ambaye kesi hiyo anaisikiliza;

atakuwa ametenda kosa la kudharau mahakama na akipatikana na hatia atastahili kupewa adhabu ya kifungo kisichozidi mwezi mmoja au faini isiyopungua shilingi laki mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(3) Endapo kitendo cha dharau kimefanywa mbele ya Mahakama, haitakuwa lazima kwa Mahakama kutoa taarifa ya kumtaka mshtakiwa kueleza sababu, lakini Mahakama itahakikisha kwamba mtu anayetuhumiwa kudharau Mahakama analifahamu kosa lake, anapewa fursa ya kusikilizwa kwa kutoa utetezi wake, na kumbukumbu za mwenendo wa kesi zitatunzwa ipasavyo.

(4) Pale ambapo dharau ya Mahakama imefanywa nje ya Mahakama, taarifa ya kumtaka mshtakiwa kutoa maelezo ya kuonesha kwanini hatua au shtaka lisifunguliwe dhidi yake itatumwa kwa mtu anayetuhumiwa kufanya kosa hilo.

Ushiriki wa Wakili na Vakili

31.-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 32 cha Sheria hii, Wakili na wakala aliyeidhinishwa kisheria anaweza kuhudhuria kwa niaba ya upande wowote katika Mahakama ya Kadhi wa Wilaya, Mahakama ya Kadhi wa Rufaa, au Mahakama Kuu.

(2) Vakili na wakala aliyeidhinishwa kisheria wanaweza kuhudhuria Mahakama za Kadhi wa Wilaya na Mahakama ya Kadhi wa Rufaa pekee kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 32 cha Sheria hii.

Kukubaliwa kwa Wakili na Vakili.

32.-(1) Jjaji Mkuu anaweza, kwa kushauriana na Kadhi Mkuu, kumruhusu Wakili au Vakili kusimamia keshi katika Mahakama ya Kadhi.

(2) Wakili au Vakili atakayeruhusiwa kusimamia kesi katika Mahakama ya Kadhi atatakiwa awe na elimu na uzoefu wa sheria ya Kiislam.

(3) Jaji Mkuu anaweza kuweka utaratibu kwa Wakili au Vakili namna ya kuomba kurushusiwa kusimamia kesi katika Mahakama ya Kadhi.

Kinga kwa Makadhi na maofisa.

33.-(1) Hakuna Kadhi au mtu mwengine yeyote anayefanya kazi ya kiMahakama atakayeshtakiwa katika Mahakama yoyote kwa madai au jinai kwa jambo lolote alilolifanya au kuamuru kufanywa katika utekelezaji wa majukumu yake, iwapo liko ndani au nje ya mamlaka yake, na endapo wakati wa kufanya wajibu wake huo alikuwa anafanya kwa nia njema huku akiamini kwamba ana mamlaka ya kufanya au kuamuru kufanywa jambo hilo.

(2) Hakuna Afisa wa Mahakama yoyote au mtu mwengine mwenye wajibu wa kutekeleza hati halali au amri za Kadhi yeyote au mtu mwengine anayefanya kazi za kiMahakama atayeshtakiwa katika Mahakama yoyote kwa madai au jinai kwa kutekeleza hati au amri ambayo anawajibika kuitekeleza, na endapo imetolewa na mamlaka au mtu anayehusika.

Kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na kubakiza.

34.-(1) Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 inafutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985, mambo yote na kesi zote zinazoendelea katika Mahakama yoyote ya Kadhi chini ya masharti ya Sheria iliyofutwa, zitaendelea kusikilizwa na kutolewa uamuzi na uamuzi na amri zilizotolewa chini ya Sheria hizo zitaendelea.

(3) Uamuzi au amri yoyote ya Mahakama yoyote ya Kadhi ambayo itakuwa haijatekelezwa au kutiliwa nguvu kabla ya Sheria hii kuanza kutumika, inaweza kutekelezwa na kutiliwa nguvu kama vile ni uamuzi au amri ya Mahakama iliyotolewa chini ya Sheria hii.

(4) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Na. 3 ya 1985, mambo na maamuzi yote yalivyofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, yatachukuliwa kuwa yamefanywa chini ya Sheria hii.

(5) Bila kujali sharti lolote chini ya Sheria hii, Makadhi waliopo wataendelea kushikilia ofisi zao.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na kutunga Sheria itakayoanzisha upya Mahakama ya Kadhi ya Zanzibar. Wazo la kuja la muundo mpya wa Mahakama ya Kadhi limeanzia katika taarifa ya utafiti uliofanya na mshauri elekezi mwaka 2013. Katika taarifa hiyo, imeonekana kwamba, jamii ya Zanzibar imepoteza imani na uaminifu kwa Mahakama ya Kadhi kutokana na utoaji haki katika Mahakama hizo kuonekana unamapungufu mengi. Mahakama ya Kadhi iliyopo sasa inaonekana haijitegemei, na inafanya kazi kama idara ya Mahakama Kuu.

Hivyo, Taarifa ya utafiti pamoja na mambo mengine imependekeza kwamba, Mahakama ya Kadhi iwe na uongozi wake tofauti na uongozi wa Mahakama nyengine za kawaida. Mahakama mpya ya Kadhi itakuwa iwe na Mrajis wake ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama. Mahakama ya Kadhi iwe na muundo mpya itakayoongozwa na Kadhi Mkuu akisaidiwa na Naibu Kadhi Mkuu. Mamlaka ya utendaji ya Kadhi na Naibu Kadhi Mkuu ni katika rufaa ambapo uamuzi wao utapelekwa

Mahakama Kuu ambao rufaa itazikilizwa na Jaji wa Mahakama Kuu ambaye lazima awe Muislam mwanamme atakayekaa na Ulamaa wane watakaoteuliwa na Mrajisi kwa mapendekezo kutoka Baraza la Ulamaa na ambao lazima wawe wataalam wa Kiislam. Uamuzi wa Mahakama Kuu utakuwa ndio wa mwisho na hakutakuwa na rufaa zaidi ya hapo.

Mbali ya hapo, kutakuwa na Mahakama za Kadhi wa Wilaya katika kila Wilaya zote Unguja na Pemba ambazo itaongozwa na Kadhi wa Wilaya husika. Mamlaka ya asili ya Kadhi wa Wilaya ni kwa mambo yote yanayotokana na malalamiko ya ugawaji wa mali zilizotokana na ndoa kwa misingi ya dini ya Kiislaam. Mamlaka kwa mambo ya fedha, ni kwa mambo yanayohusu matunzo ya familia bila ya kuweka mipaka. Mahakama ya Kadhi imepewa uwezo wa kutoa adhabu kwa mtu atakayefanya dharau kwa Mahakama kama ilivyo kwa mahakama nyengine za kawaida. Sifa za Makadhi zimeongezwa kwa maana kwamba mtu anayefaa kuteuliwa kuwa Kadhi anatakiwa awe shahada ya sheria ya mambo ya Kiislam na hasa Usulul fiqhi.

Mswada huu umegawika katika Sehemu Nne.

Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambapo imeeleza jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika ndani yake.

Sehemu ya Pili inahusu kuanzishwa, mamlaka na uongozi wa Mahakama ya Kadhi. Katika sehemu hii, masharti kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi, mamlaka ya Mahakama ya Kadhi, kutumika kwa sheria na kanuni za ushahidi, kanuni na taratibu za Mahakama ya Kadhi, uteuzi wa Kadhi na Naibu Kadhi Mkuu, uteuzi wa Kadhi wa Wilaya, Muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu, juteuzi wa Mrajis wa Mahakama ya Kadhi, lugha ya Mahakama ya Kadhi, Bajeti na fedha za Mahakama ya Kadhi na mambo mengine yameelezwa.

Sehemu ya Tatu inahusu masharti ya Usuluhishi, ambapo pamoja na mambo mengine mambo kama uamuzi wa msuluhishi, kuwasilisha kesi kwa Msuluhishi, uwezo wa Msuluhishi, haki ya wahusika na kesi ya usuluhishi, siri katika usuluhishi, muda wa usuluhishi, kufuta usuluhishi, na mazingira ambapo usuluhishi utashindikana.

Sehemu ya Nne inahusu mambo ya jumla ambapo imejumuisha masharti kuhusu uwezo wa Mahakama kutoa adhabu kwa mtu atakayeidharau mahakama, kuhudhuria kwa Wakili na Vakili katika Mahakama ya Kadhi na kufuta Sheria Nam. 3 ya 1985 na kubakiza mambo yaliyokwishafanywa chini ya sheria hiyo.

ZANZIBAR.
20 Aprili, 2017.

(HAROUN ALI SULEIMAN)
Waziri wa Nchi (AR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

)